

02.04.2026

**TANGAZO LA ZABUNI YA USOMBAJI WA KAHAWA KUTOKA GHALA LA KEMONDO
HADI TANGA/DAR ES SALAAM MSIMU 2026/2027**

Zabuni na: KCU/CN/2026/2027/04

1. KCU (1990) LTD inakaribisha zabuni ya wasafirishaji wenye magari makubwa (Malori) kwa ajili ya kusomba kahawa kutoka ghala la Kemondo kwenda Tanga/Dar es salaam kwa msimu 2026/2027.
2. Maombi yanakaribishwa kutoka kwa wenye magari yenye uwezo wa kubeba tani Zaidi ya 15 na magari ni yale yaliyofunikwa sehemu yote ya kubeba mzigo (Box Board Truck).
3. Mwombaji ataje bei ya kubeba kahawa kwa tani kwa kilometa. (Bei ieleze kama ni pamoja na VAT au bila VAT)
4. Mwombaji sharti ataje kwa kila gari; aina ya gari, uwezo wake wa kubeba mzigo.
5. Mwombaji aambatishe nakala ya leseni ya biashara, TIN, VAT pamoja na LATRA.
6. Mwombaji aeleze usalama wa mzigo utakavokuwa wakati akisafirisha kahawa hadi Tanga/Dar es salaam.
7. Wamiliki/waendeshaji aambatishe nakala ya kusajiliwa kwa mujibu wa sheria ya makampuni.
8. Mwombaji aambatishe nakala zinaonesha vielelezo vya kazi alizowahi kufanya.
9. Mwombaji aorodheshe namba za magari yatakayohusika na usombaji/usafirishaji wa kahawa.
10. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 200,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kupitia A/C Namba **01J1055955002 General A/C**.
11. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo 3-10 vilivyo tajwa hapo juu.
12. Bahasha ya maombi ifungwe vizuri kwa Lakiri na kuandikwa juu yake:- **"MAOMBI YA ZABUNI YA USOMBAJI WA KAHAWA KUTOKA GHALA LA KEMONDO HADI TANGA/DAR ES SALAAM MSIMU 2026/2027"** kwa anwani tajwa hapa chini,
MENEJA MKUU,
KCU (1990) LTD,
P.O BOX 5,
BUKOBA.
13. Bahasha hiyo iletwe kwa mkono katika Ofisi ya Manunuzi KCU kabla au mnamo tarehe 20.04.2026 saa 4.00 asubuhi siku ya Jumatatu na ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika sherehe ya ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni.
14. Maombi yatakayochelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.
Imetolewa na;

